# 3 KISIMA safi sana chatoka msalaba

1. Kisima safi sana chatoka msalaba, Kimetufungukia, chatusafisha vema.
Twaweza kusikia sauti yake Yesu: ‘’Unifuate sasa kwa kiti cha neema!’’

> ***Refrain:***
>
> *Kisima cha msalaba, Damu ya Yesu Kristo, Chatusafisha sisi sote na dhambi na hatia.*

2. Ufike, mwenye dhambi, krisima ni karibu! Uache dhambi zako,
upumzike hapa! Katika damu yake kabisa utapona,
Tazama msalaba, kisima kitokako!

3. Kisima hicho safi cha damu ya Mwokozi kinatutia
afya na nguvu ya kushinda. Mfalme wetu, Yesu, tumhimidi tena!
Furaha yetu yote ni kushukuru Mungu!

---